TANGAZO LA SERIKALI Na. 810 la tarehe. 13/9/2024

SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI,
(SURA YA 44)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 64)*

## KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UKUSANYAJI NA UCHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI ZA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 349 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi za mwaka 2023, ambazo zimerejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 4(3) kwa kufuta aya ya (c) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

> "(c) taarifa nyingine yoyote inayohusiana kadiri Tume itakavyohitaji baada ya kupokea maombi.".

Marekebisho ya kanuni ya 9

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9(2) kwa kuongeza maneno "kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika" baada ya maneno "Tume itakavyoelekeza" yaliyopo katika aya (e).

Marekebisho ya kanuni ya 20

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 20(2) kwa kufuta aya ya (i) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

> "(i) taarifa nyingine yoyote inayohusiana kadiri itakavyohitajika na Tume baada ya kupokea maombi.".

*GN. NO.810 (Linaendelea.)*

Marekebisho ya kanuni ya 27

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 27 kwa kufuta na kuandika upya aya (i) kama ifuatavyo:

"(i) kuhifadhi taarifa binafsi nyeti sehemu tofauti na zinapohifadhiwa taarifa nyingine binafsi;".

Dodoma
6 Septemba, 2024

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekno ojia ya Habari*